MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA TAREHE 27-28/07/2017 ROBO YA NNE (APRIL - JUNE).

A: WAJUMBE WALIOHUDHURIA:

1.	Mh. Namkulya S. Namkulya	-Kata ya Mihambwe	-Mwenyekiti
2.	" Makuyeka B. Salum	-Kata ya Chikongola	-M/Mwenyekiti
3.	" Katani A. Katani	-Mbunge- Tandahimba	-Mjumbe
4.	" Issa Nasoro Kalumbe	-Kata ya Mahuta	"
5.	" Ngerezani Bakari Musa	-Kata ya Kitama	"
6.	" Kawasaki Lipangati	-Kata ya Mnyawa	"
7.	" Simba Nasoro Hashimu	-Kata ya Naputa	"
8.	" Chimale S. Abdallah	-Kata ya Lukokoda	"
9.	" Sharafi Dihoni Hamisi	-Kata ya Malopokelo	"
10.	" Mtimbuka K.Ramandani	-Kata ya Nambahu	"
11.	" Mawazo S. Mbombenga	-Kata ya Nanhyanga	"
12.	" Jamali M.Mtima	-Kata ya Namikupa	"
13.	" Ally D. Nantindu	-Kata ya Michenjele	"
14.	" Nembo H. Mchola	-Kata ya Maundo	"
15.	" Ahmadi A. Ndende	-Kata ya Mkoreha	"
16.	" Ashura m. Ngope	-Kata ya Mchichira	"
17.	" Mohamedi T. Ussi	-Kata ya Kwanyama	"
18.	" Selemani Y. Chambengela	-Kata ya Litehu	"
19.	" Ismail S. Chipoka	-Kata ya Ngunja	"
20.	" Zainabu H. Mpota	-Kata ya Mkonjowano	"
21.	" Alafa T. Nakatanda	-Kata ya Mkwiti	"
22.	" Ayubu Mohamedi	-Kata ya Lyenje	"
23.	" Rashidi N. Mtima	-Kata ya Chingungwe	"
24.	" Mfaume H. Abdallah	-Kata ya Miuta	"
25.	" Mkwahe M. Milembu	-Kata ya Chaume	"
26.	" Salumu A. Mnyongo	-Kata ya Dinduma	"
27.	" Abdallah H. Ponela	-Kata ya Luagala	"
28.	" Likapa J.Nangololo	-Kata ya Mndumbwe	"
29.	" Hamisi B. Nayowela	-Kata ya Tandahimba	"
30.	" Fakihi M. Mwango	-Kata ya Mdimba	"
31.	" Yusufu B. Nampoto	-Kata ya Mkundi	"
32.	" Asha R. Tebwa	-Viti Maalum	"
33.	" Halima Tamatama	-Viti Maalum	"
34.	" Huduma S. Mnoda	-Viti Maalum	"
35.	" Amina Issa Mpota	-Viti Maalum	"
36.	" Hadija S. Mnihwika	-Viti Maalum	"
37.	" Shamia M. Kaisi	-Viti Maalum	"
38.	" Fidea A. Hittu	-Viti Maalum	"
39.	" Asia A. Likoba	-Viti Maalum	"

40. "	Rehema C. Liute	-Viti Maalum	"
41. "	Hawa M. Ramandani	-Viti Maalum	"
42. "	Amina A. Simba	-Viti Maalum	"

B: WASIOFIKA

1.	Mhe. Ramadhani Ulaya	-Kata ya Milongodi	Amefariki

C:WAKUU WA IDARA NA VITENGO WALIOHUDHURIA

1.	Ndg Said A. Msomoka	- Mkurugenzi Mtendaji (W)	Katibu
2.	Ndg. Ahmada Suleiman	- Afisa Utumishi (W)	
3.	" Machela A.H	-Mweka Hazina (W)	
4.	" Issa Naumanga	-Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W)	
5.	Eng: Paul Mlia	-Mhandisi wa Ujenzi (W)	
6.	" Esther Masele	- Kaimu Mhandisi wa Maji (W)	
7.	Dr. Edmond Mmuni	-Kaimu Mganga Mkuu (W)	
8.	Ndg: Bibiana Molenga	-Kimu Afisa Maendeleo ya Jamii(W)	
9.	" Hadija Mwinuka	- Afisa Elimu Msingi(W)	
10.	" Robert Mwanawima	- Afisa Mifugo na Uvuvi (W)	
11.	" George Kashura	- Kaimu Afisa Uchaguzi(W)	
12.	" Sostheness Luhende	-Afisa Elimu Sekondari (W)	
13.	" Judicy Mnizava	- Kaimu Afisa Mipango (W)	
14.	" William Kongola	-Mkaguzi wa ndani wa Hesabu(W)	
15.	" Nasibu Shaibu	- Kaimu Afisa Ardhi na maliasiri(W)	
16.	" Nosyaga Mwailunga	- Kaimu Afisa Usafi na Mazingira(W)	
17.	" Rajabu C. Athman	-Afisa Utamaduni	
18.	" Soud Said	- Afisa Ushirika	
19.	" Zuberi Sarahani	-Mwanasheria	
20.	" Protas Muhanuzi	-Afisa Manunuzi(W)	
21.	" Ismaely Mbilinyi	-Mratibu wa TASAF	
22.	" James C. Chitumbi	-TEO Tandahimba	
23.	" Rajabu Lwazi	- TEO- Mahuta	
24.	" Violeth Mahembe	- Mratibu wa CHF	
25.	" Kashen Mtambo	- Afisa Mipango	

D: WAALIKWA

1.	Mh. Sebastian Waryuba	-Mkuu wa Wilaya Tandahimba
2.	Ndg: Mohamed Wasinde	-Afisa Serikali za Mitaa(M)
3.	Ndg: Thomas Mhecha	-Afisa Usalama (W)
4.	" Mohamedi Mtama	- Mshauri wa Mgambo(W)
5.	" Faki o. Said	-Kny: Mkuu wa Polisi(W)
6.	" Benson Lulandala	-Kny:Kamanda wa TAKUKURU(W)
7.	" Rymond Mapunda	- Kaimu Afisa Uhamiaji(W)
8.	" Juma A. Lusasi	-Afisa Tarafa Mahuta
9.	" Rehema Hoza	-Afisa Tarafa Litehu

10. " Born Minga -Afisa Tarafa Namikupa
11. " mbaraka Hittu - Katibu CUF(W)
12. " Willy Mkapa -Katibu CHADEMA (W)
13. " Namtula A. Haji - Mwenyekiti CCM(W)
14. " Domina A. Soko -Katibu CCM (W)
15. " Ally S. Muwanya -Mwenyekiti wa Mji Mdogo Tandahimba

E: SEKRETARIATI

1. Christian Mazuge
2. Sofia Nanjota
3. Mohamedi Namkuva

MUHT.NA. 44/2016/2017- KUFUNGUA MKUTANO

Kabla ya kikao kufunguliwa wimbo wa Taifa uliimbwa na kusoma dua ya kuiombea Halmashauri. Katibu aliwakaribisha wajumbe na waalikwa wote kikaoni. Alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti alifungua kikao kikao saa 5: 01 asubuhi.

MUHT.NA. 45/2016/2017- KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO

Agenda kumi na moja (11) ziliwasilishwa mbele ya wajumbe wa kikao kwa ajili ya kuzipitia. Baada ya kuzipitia wajumbe waliridhia agenda hizo ambazo ni:-

SIKU YA KWANZA YA BARAZA TAREHE 27/04/2017

1. Kufungua kikao cha Baraza la Madiwani
2. Kuthibitisha agenda za kikao cha Baraza la Madiwani
3. Kupitia taarifa mbalimbali za miradi ya maendeleo ya Kata

SIKU YA PILI YA BARAZA TAREHE 28/04/2017

4. Kujibu maswali ya Wahe. Madiwani ya papo kwa papo
5. Kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 27-28/04/2017.
6. Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
7. Kujibu maswali ya Waheshimiwa Madiwani ya Maandishi
8. Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya kipindi cha Robo ya nne (Aprili - June 2017).
9. Taarifa mbalimbali za kamati za kudumu za Halmashauri ya Wilaya
    a) Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi
    b) Kamati ya Elimu, Afya na Maji
    c) Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
    d) Kamati ya Kudhibiti UKIMWI
10. Uchaguzi wa Makamu mwenyekiti wa Halmashauri na kamati za kudumu za Halmashauri.
11. Mapendekezo ya Ratiba ya vikao vya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

12. Taarifa za Kiutumishi
13. Kufunga kikao.

MUHT.NA. 46/2016/2017-KUPITIA TAARIFA MBALIMBALI ZA MIRADI YA MAENDELEO YA KATA,

Waheshimiwa madiwani waliwasilisha taarifa ya miradi ya maendeleo kutoka katika kata zao. Wajumbe walizipokea taarifa hizo.Taarifa hizo zimewekwa katika kitabu kimoja katika kumbukumbu za Halmashauri. Kata zilizowasilisha taarifa ni,

1. Mahuta
2. Malopokelo
3. Michenjele
4. Luagala
5. Ngunja
6. Miuta
7. Mnyawa
8. Namikupa
9. Chikongola

MJADALA

Mjumbe alihoji kwa nini matokeo ya kidato cha sita Shule ya Sekondari Tandahimba yameshuka kutoka nafasi ya 10 kitaifa hadi ya 33 kitaifa.

Mjumbe mwingine alihoji juu ya upatikanaji wa nyumba za walimu.

Mkurugenzi alieleza kuwa suala la kushuka kwa matokeo ya kidato cha sita Tandahimba Sekondari, wadau wamekutana hivyo majibu yatatolewa kwenye taarifa za kamati.

Afisa Elimu Sekondari(W) alieleza kuwa wanafunzi wote wa kidato cha sita wamefaulu na wana sifa za kujiunga na vyuo vikuu ila imeshuka kutoka nafasi ya 10 kitaifa hadi ya 33 kitaifa kwani nafasi inatokana na ushindani kati ya shule zilizokuwa na wanafunzi wa kidato cha sita waliofanya mitihani.

Changamoto zilizopo katika shule ya Sekondari Tandahimba ni upungufu wa vitabu na kutokuwepo na maktaba. Mwenyekiti alieleza kuwa kuna haja ya kuunda kamati na kuchunguza changamoto zinazoikabili shule ya Sekondari Tandahimba.

Katibu alieleza kuwa kuna umuhimu wa kuunda kamati itakayobaini changamoto zilizosababisha matokeo ya kidato cha sita kushuka na kuomba ushirikiano katika kutatua changamoto hizo.

SUALA LA HUDUMA YA UPASUAJI

Mjumbe aliuliza kwa nini huduma ya upasuaji katika Kituo cha Afya Mahuta imesimama.

Ilielezwa kuwa kusimama kwa shughuli za upasuaji katika kituo cha Afya Mahuta, limetokana na watumishi waliopatwa na sakata la vyeti feki, Mwenyekiti aliwasihi Madiwani kuwa wavumilivu kwani idara nyingi zimepata upungufu wa watumishi.

Suala la huduma za Afya Mahuta kukosa huduma ya upasuaji Katibu aliahidi kulifanyia kazi kwa kutoa huduma za upasuaji angalau mara mbili za wiki.

MAELEZO YA MKUU WA WILAYA.

Mkuu wa Wilaya aliwapongeza madiwani kwa taarifa zinazojadili maendeleo ya kata. Alisisitizaa kila kata kutilia umuhimu ya suala la viwanda na biashara katika ngazi ya kata.

Alieleza kuwa Mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa taarifa ya viwanda na biashara kuwa ni:-

Idadi ya wafanyabiashara,Maeneo ya viwanda yaliyotengwa,Changamoto zinazojitokeza na namna zinavyotatuliwa.

Alieleza kuwa kata ya Malopokelo ina eneo la viwanda ambalo haliendelezwi na kushauri wasiondeleza maeneo hayo wanyang'anywe.

Alieleza kuwa suala la kushuka kwa matokeo ya kidato cha sita, alifafanua kuwa kuna haja ya kujua changamoto za shule ya sekondari Tandahimba ili matokeo yaendelee kuwa mazuri.

Katibu alimkalibisha Mwenyekiti aahirishe mkutano kwa siku ya kwanza. Mwenyekiti alisistiza madiwani kuwahimiza watendaji kuingiza masuala ya viwanda na biashara kwenye taarifa zao za kila robo na kuwasilisha taarifa hizo siku moja kabla ya kikao kwa katibu wa kamati saa sita mchana (siku ya mkutano wa chama) na asiyefanya hivyo asilipwe posho. Mwenyekiti aliahirisha Kikao muda wa saa 06:16 mchana.

SIKU YA PILI TAREHE 28.07 2017 BARAZA LA MADIWANI.

Katibu alimkaribisha Mwnyekiti aendeleze kikao. Mwenyekiti aliendeleza kikao saa 11:07 asubuhi.

MUHT.NA. 47/2016/2017- KUJIBU MASWALI YA WAHE. MADIWANI YA PAPO KWA PAPO

Wajumbe walipewa nafasi ya kuuliza maswali ya papo kwa papo. Maswali yaliyoulizwa ni kama ifuatavyo:-

Mh. Abdallah H. Ponela Diwani wa Kata ya Luagala,alihoji kama kuna kikao chenye mamlaka ya kutengua maamuzi ya kikao cha baraza la madiwani Mwezi Januari ya kuanzisha shule za sekondari za kidato cha sita katika kila Tarafa ambapo kwa tarafa ya Litehu ilichaguliwa shule ya Luagala na baadae kupandishwa na kupelekwa shule ya sekondari Ngunja.

Mh. Hawa Ramadhani Diwani Viti Maalum aliuliza Halmashauri ina mpango gani wa kununua gari za kuzolea taka.

Kuna mikakati gani ya kusaidia kata ya Tandahimba kimapato kwani vyanzo vyote vipo chini ya Halmashauri.

Mh. Sharafi Dihoni Hamisi Diwani wa Kata ya Malopokelo Aliuliza ni kwa nini Mamlaka ya Mji mdogo haifanyi kazi ?

MAJIBU

Katibu alieleza kuwa Mji mdogo wa Tandahimba umeanza kufanya kazi tatizo lililopo ni majengo ya ofisi na aliahidi kulifanyia kazi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Katibu aliahidi Gari la taka litanunuliwa trekta na tela kwa ajili ya kuzolea taka kwa 2017/2018.

Swali la nyongeza.

Mh: Hamisi B. Nayowela Diwani wa Kata ya Tandahimba aliomba Mwenyekiti na katibu wakutane na wenyeviti wa vitongoji ili kusikiliza changamoto zinazowakabili.

JIBU: Katibu aliahidi kukutana na wenyeviti wa vitogoji.

MUHT.NA. 48/2016/2017- KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 27-28/04/2017

Muhtasari wa kikao cha Baraza la madiwani vya tarehe 27-28/04/2017 uliwasilishwa kwa ajili ya kuupitia na kuuthibitisha. Mara baada ya wajumbe

kuusoma muhtasari huo, walikubali kuwa vilivyoandikwa ni kumbukumbu sahihi za kikao hicho.

MUHT.NA. 49/2016/2017- TAARIFA YA MKURUGENZI MTENDAJI (W)
Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa yake mbele ya wajumbe wa kikao. Taarifa hiyo ilieleza mambo yafuatayo:-

Katibu alieleza kuwa katika kipindi cha Aprili – June 2017, Halmashauri imefanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo katika Nyanja mbalimbali.

ZOEZI LA UHAKIKI WA WATUMISHI
Halmashauri iliendelea kutekeleza maagizo mbalimbali ya serikali likiwemo zoezi la uhakiki wa watumishi wake. Katika zoezi hili watumishi 57 wameachishwa kazi mwezi Mei, 2017 kutokana na kughushi vyeti vyao vya taaluma. Watumishi hao wametoka idara mbalimbali kama ifuatavyo idara ya Afya 33,Idara ya Elimu Msingi 17, Idara ya Utawala 4, Idara ya Fedha na Biashara 1 na idara ya Kilimo Umwagiliaji na Ushirika 2.

WATUMISHI WALIOSIMAMISHIWA MSHAHARA KWA KUKOSA SIFA.

Jumla ya watumishi 28 wamesimamishiwa mshahara kuanzia mwezi Julai 2017 kwa maagizo ya serikali kutokana na kukosa sifa za kimuundo za kuajiriwa katika utumishi wa umma baada ya tarehe 20, mei,2004. Kwa mujibu wa nyaraka za miundo ya Utumishi wa Umma watumishi walioajiriwa tarehe 20,mei 2004 walitakiwa kuwa na vyeti vya ufauku wa kidato cha nne.

UPATIKANAJI WA PEMBEJEO.

Wilaya ya Tandahimba inakadiriwa kuwa na miti ya Korosho 7,452,803 na inayohudumiwa ni 5,156,414. Takwimu hizi za mikorosho zinatoa taswira ya kuhitaji tani 6500 ya salfa ya Unga.

Mgao wa pembejeo ambao Halmashauri ya Tandahimba ilipata msimu wa 2017/2018 ni tani 4,717 salfa ya unga ,lita 86,471 viatirifu vya maji na mabomba 326. Hadi tarehe 24/07/2017 ilikuwa imepokelewa kiasi cha tani 2,745.8 salfu ya unga, na lita 60,268 za viatilifu vya maji. Kuchelewa kufika kwa pembejeo imesababisha changamoto ya upatikanaji wa pembejeo na kusababisha kupanda kwa bei na kufika Tsh. 70,000/= kwa kilo 25 za ulfa ya unga.

UREJESHAJI WA MICHANGO YA PEMBEJEO KWA WAKULIMA

Kufuatia uamuzi wa serikali wa kutoa bure pembejeo kwa mkulima kiasi cha shilingi 2,175,400,750/= zilizokusanywa kutoka kwa wakulima zimerejeshwa kwa wakulima ili waweze kununua pembejeo wenyewe kwa kuwa pembejeo ya ruzuku haikidhi mahitaji ya wakulima.

MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA

Wanafunzi waliofanya mtihani mwezi mei 2017 walikuwa 50 na wanafunzi wote wamefauli kwa madaraja yafuatayo daraja la kwanza 13, daraja la pili 34, daraja la tatu 3 na hakuna mwanafunzi aliyepata daraja la nne wala ziro. Shule kimkoa ilishika nafasi ya pili na kitaifa nafasi ya 33.

TAARIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ilielezwa kuwa kwa mujibu wa taarifa ya mkaguzi na mdhibiti Mkuu wa Hesabu za serikali kwa mwaka wa fedha uliomalizika June, 2016, Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ilipata hati safi katika hesabu za Jumla pamoja na miradi ya Afya,maji, barabara na kilimo,umwagiliaji na mifugo.

Taarifa ilipokelewa.

MUHT.NA. 50/2016/2017- KUJIBU MASWALI YA WAHE. MADIWANI YA MAANDISHI
Maswali ya maandishi hayakuwasilishwa.

MUHT.NA.51 /2016/2017 –TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA NNE (APRILI- JUNI, 2017)
Kaimu Afisa Mipango alieleza kuwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba imeidhinishiwa kupokea na kutumia jumla ya shilingi 8,978,587,000.00/= katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kuzingatia , Dira ya maendeleo ya taifa ya mwaka 2025 (vision 2015), Sera mbalimbali za kisekta pamoja na malengo ya maendeleo endelevu (SDG's). Hii ni kutokana na dira na dhima ya Halmashauri kwamba**"*Ifikapo 2018 halmashauri ya wilaya ya Tandahimba , kwa kutumia rasilimali zilizopo, utaalam na ushirikishaji wa jamii, iwe imetoa huduma bora kujenga uchumi endelevu utakaowezesha maisha bora ya wananchi*"**

Fedha hizo zilitarajiwa kuchangiwa na wadau mbalimbali ikiwemo mapato ya ndani ya Halmashauri (Ownsource), ruzuku ya maendeleo toka serikali kuu (LGCDG), mfuko wa barabara (Road Fund), mfuko kabambe wa afya (health Sector Basket Fund), mfuko wa maji (RWSSP), mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari (Word Bank), Mpango wa maendeleo Elimu Msingi(PEDP), EGPAF, Mfuko wa Jimbo, Pamoja na mfuko wa maendeleo ya jamii (TASAF).
Mchanganuo wa fedha hizo kwa wachangiaji hapo juu kwa mwaka 2015/2016 ni kama unavyoonekana kwenye jedwali hili:-

NA	CHANZO/MCHANGIAJI	MAKISIO	FEDHA TOLEWA	FEDHA TUMIKA	FEDHA ZISIZOPOKELEWA	% YA FEDHA POKELEWA
1	OWNSOURC	3,304,250,000	2,653,418,376	2,653,418,376	650,831,624.00	80.3

	E	.00	.00	.00		
2	LGCDG	818,851,000.00	286,338,000.00	286,338,000.00	532,513,000.00	34.97
3	MFUKO WA MAJI (NRWSSP)	964,000,000.00	736,390,368.69	691,846,257.00	227,609,631.31	76.39
4	ROAD FUND	1,222,290,000.00	886,247,696,06	762,050,903.00	336,042,303.94	72.51
5	BASKET FUND	484,556.000.00	484,556.000.00	464,608,762.00	0.00	100.00
6	PEDP	100,000,000.00			100,000,000.00	0.00
7	MFUKO WA JIMBO	46,991,000.00	43,252,000.00	43,094,000.00	3,739,000.00	92.04
8	TASAF	1,459,485,000.00	1,472,460,342.12	1,472,460,342.12	-12,975,342.12	100.89
9	WORD BANK	578,164,000.00			578,164,000.00	0.00
	JUMLA	**8,978,587,000.00**	**6,562,662,782.87**	6,373,816,640.12	**2,415,924,217.13**	**73.1**

Hadi kufikia tarehe 30/06/2017, Halmashauri ilikuwa imepokea na kutumia jumla ya shilingi **6,562,662,782.87 na kutumia jumla ya shilingi 6,362,687,990.12 katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo** sawa na asilimia 73.1 ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2016/2017

Aidha kupitia mfuko wa maendeleo ya jamii TASAF katika robo ya nne Halmashauri ilipokea jumla ya Tshs. 392,612,000.00 na kutumia jumla Tshs. 391,048,000.00 kwa ajili ya malipo ya kaya masikini. Hata hivyo Tshs. 1,564,000.00 zimerejeshwa TASAF Makao Makuu kutokana baadhi ya walengwa kukosa sifa za kulipwa fedha hizo kutokana na vifo au kuhama makazi.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri imepokea shilingi 21,815,810.76 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya P4R kwa shule 7 za msingi, kwa shule za sekondari, Halmashauri imepokea shilingi 25,782,322.18 kwa shule 2.
Taarifa ilipokelewa.

MJADILIANO
USHAURI
Mjumbe alishauri kuwa katika kuandaa taarifa ya miradi kuna miradi imejirudia hivyo marekebisho yafanyike.

MASWALI

Mjumbe alihoji sababu za kuingiziwa fedha pungufu mradi wa kumalizia madarasa shule ya Msingi Namikupa 1.

Mjumbe alihoji juu ya barabara ya Mikunda-Ngongo umeoneshwa imekamilika wakati haujatekelezwa.

Mjumbe alihoji Ukamilishaji wa nyumba ya kata Chaume inaonesha fedha zinatafutwa na mwaka wa fedha umeisha 2016/17.

Mjumbe alihoji barabara ya Mivanga-Nambahu-Mkola-Mikuyu-Mkula zinaonesha zimefanyiwa kazi ila kiuhalisia hazijafanyiwa kazi.

MAJIBU.

Ilijibiwa kuwa ujenzi wa Nyumba ya Mtendaji Chaume haukutekelezwa kwa kuwa ulikuwa kwenye mapato ya serikali kuu na kwa 2017/18 miradi hiyo imewekwa kwenye mapato ya ndani.

Mradi wa madarasa 2 shule ya msingi Namikupa 1 mradi huo ulibadilishwa kutokana na tatizo la vyoo kwa ridhaa ya vikao vya Halmashauri.

Mwenyekiti aliongeza kwa kufafanua kuwa miradi mingi ya mapato ya serikali kuu haijatekelezwa ila mapato ya ndani imetekelezwa.

USHAURI

Mjumbe alishauri miradi ya ujenzi wa vyoo itolewe kwa uwiano kwenye shule zote na miradi ambayo haijatekelezwa ibainishwe.

Mjumbe alihoji kutengewa fedha kidogo milioni 6 kwa mradi wa machinjio kwani hazitoshi kukamisha mradi.

JIBU: Ilielezwa kuwa mradi haujakamilika, mradi huo utaendelea kutekelezwa kwenye bajeti ijayo 2018/2019.

MUHT.NA. 52/2016/2017- TAARIFA MBALIMBALI ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA

I. KAMATI YA FEDHA, MIPANGO NA UONGOZI

Mwenyekiti wa kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi aliwasilisha taarifa hiyo mbele ya wajumbe wa kikao. Taarifa ilieleza jinsi kamati ya fedha ilivyofanya vikao na agenda zilizojadiliwa. Pamoja na taarifa, iliambatanishwa mihtasari ya vikao vya kamati hiyo na taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi June, 2017.
Taarifa ilipokelewa.

II. KAMATI YA ELIMU,AFYA NA MAJI

Mwenyekiti wa kamati ya Elimu, Afya na Maji aliwasilisha taarifa ya kamati hiyo mbele ya wajumbe wa kikao. Taarifa ilieleza jinsi kamati ya Elimu, Afya na Maji ilivyofanya vikao vyake. Pamoja na taarifa, uliambatanishwa muhtasari wa kikao cha kamati hiyo cha tarehe 06/04/2017.
Taarifa ilipokelewa

III. KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA

Mwenyekiti wa kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira aliwasilisha taarifa iliyoeleza jinsi vikao vya kamati hiyo vilivyofanyika. Pamoja na taarifa, uliambatanishwa muhtasari wa kikao cha kamati hiyo cha tarehe 07/04/2017.

Taarifa ilipokelewa

IV. KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI

Mwenyekiti wa kamati ya Kudhibiti UKIMWI aliwasilisha taarifa hiyo mbele ya wajumbe wa kikao.Taarifa ilieleza jinsi kamati hiyo ilivyofanya vikao vyake. Pamoja na taarifa, uliambatanishwa muhtasari wa kikao cha kamati hiyo wa tarehe 06/0/2017.
Taarifa ilipokelewa.

MUHT.NA. 53/2016/2017: UCHAGUZI WA MAKAMU MWENYEKITI WA HALMASHAURI NA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI.

Kabla ya uchaguzi kuanza katibu aliwasilisha taratibu za kuunda kamati za kudumu za halmashauri kuwa zinaundwa chini ya sheria ya serikali za mitaa sura ya 287. Taratibu hizo ni pamoja na.

a. Wagombea wa nafasi ya Makamu mwenyekiti kupewa nafasi ya dakika tano kujieleza na kuomba kura
b. Kila mjumbe wa Halmashauri atakuwa angalau kamati moja ya kudumu
c. Kamati zizingatie uwiano wa vyama,jinsi na uzoefu katika kamati
d. Wajumbe wa kamati za kudumu watashika nyadhifa zao kwa muda wa mwaka mmoja.

Taarifa ilipokelewa.

UCHAGUZI

Kabla ya uchaguzi kuanza Makamu Mwenyekiti aliyekuwepo alitoa neno la shukrani kwa baraza kwa kipindi chote cha uongozi na kisha alijiuzuru rasmi ili kuacha nafasi wazi.

Katibu aliwataja wagombea waliopendekezwa na vyama vyao kugombea nafasi ya makamu mwenyekiti wa Halmashauri.

1. Mh: Fakihi Makuchu Mwango - CCM
2. Mh: Jamali Mussa Mtima - CUF

Wagombea wote wawili walipewa nafasi ya kujieleza na kuomba kura kwa wajumbe.

Wagombea walichagua mawakala wao ambao walikagua masanduku pamoja na karatasi za kupigia kura.

Zoezi la kupiga kura lilifanyika ambapo wapiga kura walipewa karatasi na kupiga kura sehemu ya siri na kisha kuweka karatasi kwenye sanduku lililo sehemu ya wazi.

KAMATI ZA KUDUMU

Wajumbe walipendekeza na kisha walikwenda sehemu na kufanya uchaguzi wa mwenyekiti wa kamati.

MATOKEO NAFASI YA MAKAMU MWENYEKITI

1. Mh: Fakihi Makuchu Mwango - CCM alipata kura 14
2. Mh: Jamali Mussa Mtima - CUF alipata kura 27

Hakuna kura iliyoharibika hivyo katibu alimtangaza **Mh: Jamali Mussa Mtima** kuwa Mshindi kwa kupata kura 27

MATOKEO NAFASI YA MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA

Jumla ya wajumbe waliopiga kura ni 18

Mheshimiwa Salumu Mnyongo kura 06

Mheshimiwa Chimale Abdalah kura 12

MATOKEO NAFASI YA MWENYEKITI WA KAMATI YA ELIMU AFYA NA MAJI

Jumla ya Wajumbe waliopiga kura ni 18

Mheshimiwa Amina Mpota – kura 7

Mheshimiwa R. Mtimbuka - kura 11

MATOKEO YA MWENYEKITI KAMATI YA MAADILI

Wajumbe waliopiga kura ni -6

Mheshimiwa Ngerezani -5 Hapana – 1

Hakuwa na Mgombea mwingine

WAJUMBE WA KAMATI YA FEDHA, MIPANGO NA UONGOZI

Baada ya kutangaza matokeo mwenyekiti alitangaza majina ya wajumbe wa kamati ya fedha ambao ni Mwenyekiti wa Halmashauri, Makamu Mwenyekiti, Mbunge wa Tandahimba, Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu afya na Maji,Mwenyekiti wa kamati ya uchumi ujenzi na Mazingira, mwenyekiti wa kamati ya maadili na wengine ni Mheshimiwa Ali Nantindu. Mheshimiwa Hawa Ramadhani, Mheshimiwa Amina Simba, Mheshimiwa Sharafi Dihoni.

Washindi walipewa nafasi ya kushukuru nao walishukuru.

MUHT.NA. 54/2016/2017 - MAPENDEKEZO YA RATIBA YA VIKAO MWAKA 2017/2018

Mapendekezo ya ratiba ya vikao vya kamati za kudumu yaliwasilishwa kwa wajumbe. Mapendekezo yaliyowasilishwa ni ratiba kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mapendekezo yalikubaliwa

MUHT.NA. 55/2016/2017 - TAARIFA ZA KIUTUMISHI

Afisa Utumishi(W) alieleza kuwa mwezi Oktoba, 2016 Halmashauri ya Wilaya Tandahimba iliendesha zoezi la uhakiki wa vyeti ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Katibu Mkuu Utumishi kwa barua yenye kumb Na. 228/290/02/05 ya tarehe 06/10/2016 iliyohusu uhakiki wa vyeti vya kidato cha nne, sita na ualimu ambapo zoezi lilifanyika kwa kushirikiana na maafisa kutoka Baraza la Mitihani ambapo walifanya uhakiki ofisi ya Katibu tawala wa Mkoa.

Zoezi hili lilikuwa ni la Kitaifa na matokeo yaliletwa 28 April, 2017 na kupokelewa na **Mhe. Rais Dokta John Pombe Joseph Magufuli** ambaye aliagiza waache kazi na waondolewe kwenye orodha ya malipo ya mishahara ya serikali (payroll).

MATOKEO YA TAARIFA YA VYETI VYA KUGHUSHI

Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba watumishi waliofanyiwa uhakiki walikuwa watumishi 54 walibainika na vyeti vya kughushi. Baada ya matokeo hayo ya zoezi la uhakiki ilitolewa fursa ya watumishi kukata rufaa wale ambao hawakurudhika na matokeo ya zoezi hilo, watumishi wote walioelekezwa taratibu za kukata rufaa na matokeo ya rufaa ni kama ifuatavyo:-

JEDWALI LA WALIOBAINIKA KUWA NA VYETI VYA KUGHUSHI

NA	KUNDI	IDADI
1	Walioghushi awali	54
2	Waliokata rufaa	3
3	Wasiokata rufaa	51
4	Walioshinda rufaa	2
5	Walioshindwa rufaa	1
6	Walioongezeka baada ya rufaa	5

Kwa mujibu wa sheria ya Utumishi wa Umma, namba 08 ya mwaka 2002, kifungu 24 Mhe. Rais aliagiza waondolewe kwenye Utumishi wa Umma. Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma za 2009, Kanuni D.12 mtumishi yeyote atakayebainika kuwasilisha taarifa za uongo kwa ajili ya kujipatia ajira atakuwa ametenda kosa na hatakuwa na sifa za utumishi wa Umma, na atachukuliwa hatua za kinidhamu na jinai.

Watumishi 55 wamepatikana na kosa la kujipatia ajira kwa njia ya udanganyifu. Kati ya hao ni walimu ambao mamlaka yao ya nidhamu ni Tume ya Utumishi wa walimu (TSC). Taarifa yao tutawasilisha katika mamlaka husika kwa ajili ya kuhitimisha ajira zao (Angalia orodha ya walimu kiambatanisho A). wenye vyeti vya kughushi angalia kiambatanisho "B" (Orodha ya watumishi wenye vyeti vye kughushi).

Taarifa ilipokelewa.

Nasaha za Mkuu wa Wilaya:

Mkuu wa Wilaya aliwapongeza waliochaguliwa kwenye Uchaguzi wa Makamu Mwenyekiti na wenyeviti wa Kamati. Alisisitiza pia umakini kwa wataalam wakati wa kuandaa miradi ya maendeleo. Alieleza kuwa wananchi wamekuwa na malalamiko kuwa miradi inatolewa kwa upendeleo kwa baadhi ya maeneo. Alisisitiza pia kuwa wananchi wapewe elimu juu ya athari ya kujenga karibu na machinjio.

SUALA LA PEMBEJEO.

Mkuu wa Wilaya alieleza kuwa asilimia 58% ya pembejeo zimesambazwa japokuwa kuna mapungufu hivyo aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kutoa ushirikiano katika kuwabaini wabadhilifu wa pembejeo.

UJIO WA MKUU WA MKOA.

Mkuu wa Wilaya alielezwa kuwa Mkuu wa Mkoa atawasili Tandahimba tar.5-7/08/2017 na kuomba madiwani na wananchi wote kutoa ushirikiano. Aliwasihi madiwani kuwahamasisha wananchi kufungua akaunti kwa ajili ya malipo ya korosho. Alisisitiza juu ya amami na utulivu kwa ajili ya Tandahimba.

Aliwaomba pia kuwa na uvumilivu kutokana na upungufu wa watumishi na kueleza kuwa atakuwa na kikao tarehe 31/07/2017 saa 2:00 asubuhi na watumishi wa umma.

MUHT.NA.56/2016/2017 KUFUNGA MUKUTANO

Katibu alimkaribisha mwenyekiti ili aweze kufunga kikao. Mwenyekiti aliwasihi walioshindwa kwenye uchaguzi kuwa wavumilivu. Aliwasihi kufanya kazi za usimamizi wa miradi. Alieleza kuwa kanuni inaruhusu Mwenyekiti kuvunja kamati kwa maslahi ya Halmashauri na kisha alifunga Mkutano saa 08:04 mchana.

MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA

JINA _____ **JINA** _____

MWENYEKITI **KATIBU**

SAINI _____ **SAINI** _____

_____

TAREHE